## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA RAIS

## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, 2023**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu.**

**Mkuu wa Shule 0757533898**

**Makamu Mkuu wa Shule 0755247496**

**Matron 0783451863**

**Shule ya Sekondari ya Wasichana Mpanda**

**S.L.P 228,**

**MPANDA- KATAVI.**

**Tarehe 12.06.2023**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA MPANDA HALMASHAURI YA MPANDA MANISPAA MKOA WA KATAVI MWAKA 2023/2024.**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka **2023/2024** na atasoma tahasusi ya …………
Shule ya Sekondari ya Wasichana Mpanda ipo umbali wa Kilometa 8 Magharibi,kutoka stendi kuu ya mabasi ya Mji wa Mpanda.Usafiri kutoka mjini kuja shuleni unapatikana.Kutoka kituo cha mabasi **Mizengo Pinda,** Nauli ni Shilingi 3000/= kwa pikipiki na Shilingi 3000/= kwa bajaji.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe **13.08.2023,**hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 13.08.2023, **Mwisho wa kuripoti ni tarehe 31.08.2023**

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni **kitambaa cha masai suzuki,mchanganyiko wa kijani na nyeusi**,mshono wa **Linda box(**moja mbele na moja nyuma,pembeni kulia na kushoto, malinda mawili**),**kwa matumizi ya darasani,iwe ndefu hadi kwenye kifundo cha miguu **(zingatia maelekezo kuepuka usumbufu wa kushona sketi mara mbili)**.Rejea kiambata **A-1** upande wa rangi ya kitamaa na aina ya mshono..

ii. Mashati mawili meupe yenye mikono mirefu.

iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni nyeupe kitambaa cha **harua**,ni sare ya darasani.Hijabu ya pili ni chekechea rangi ya **ugoro,**ni sare ya kushindia.Zote zifunike kifua cha mwanafunzi na pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.

iv. Sare ya Michezo ni sketi fupi rangi ya **Blue bahari,**kitambaa cha sukari sukari, inayofika kwenye magoti,pia awe na raba jozi moja rangi nyeusi atakayoivaa kipindi cha michezo,Traki suti moja rangi ya **Dark blue** .

v. Viatu vya shule ni vyeusi visivyo vya kufunga na kamba na visivyo na kisigino kirefu(**simple shoes**)

vi. Soksi jozi mbili nyeupe atakazo vaa wakati wa darasani na jozi mbili nyeusi atakazo vaa nje ya darasa.

vii. Sweta moja rangi ya kijani jeshi yenye nembo ya shule.

viii. Nguo za kushindia (*shamba dress*) ni Sketi moja rangi ya **Ugoro,**mshono wake ni **Linda box**,iwe ndefu hadi kwenye kifundo cha miguu **(zingatia maelekezo kuepuka usumbufu wa kushona sketi mara mbili),**rejea kiambata **A-2 ,na blauzi ni Kitambaa cha chekechea rangi ya ugoro,mshono wake ni**

**mikono mirefu shingo iwe ya duara.** upande wa rangi ya kitambaa na aina ya mshono,rejea kiambata **A-3**.

ix. Tisheti (T-shirt)

- T-shirt moja rangi ya **Dark Blue** aina ya Tujenge yenye nembo ya shule.
- T -shirt moja rangi ya **Njano** aina ya Tujenge yenye nembo ya shule..

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari Kaunta quire 3 yawe 10,madaftari 10 aina ya Msomi.
ii. **Ream** mbili(2) **(A4)** kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (Rejea kiambata **"B"**hapo chini).
iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
v. Scientific Calculator kwa tahasusi za PCB, PCM, EGM, ECA, HGE na CBG.
vi. Godoro linakodishwa shuleni kwa gharama ya **Shilingi 10,000.00** kwa mwaka;
vii. Mashuka Jozi 2 rangi ya kijani kibichi, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 rangi nyeupe.
viii. Nguo za ndani za kutosha;
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
xi. Kwanja 1, jembe 1, Brush ngumu 1, mifagio 2 wa ndani(Soft brush) na wa nje(Chelewa chelewa).

**2.3 Michango mbalimbali**

**a) Shule za Bweni**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

- Fedha zote zilipwe kwenye akaunti ya shule **61901100009 NMB.** Jina la akaunti **MPANDA GIRLS SECONDARY SCHOOL.**

- **Kwa mwanafunzi asiye na BIMA ya afya,akatiwe Bima ya afya au aje na Tsh 50,400/= (cash),kwa ajili ya kumkatia Bima ya afya ili kuepuka usumbufu pindi mwanafunzi atakapo ugua(muhimu)**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- ❖ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (**Medical Examination Form**) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;(**Kiambata "C"**)
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;(**Kiambata "D"**)
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; (**Kiambata "E"**)na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

## KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

# "MAISHA NI KUJIFUNZA"

**Saini ya Mkuu wa Shule** ....Sabas....

**Jina la Mkuu wa Shule** ..NYABISE M. SABASI..

**Mhuri wa Mkuu wa Shule** ..... MKUU WA SHULE Shule ya Sekondari ya Wasichana Mpanda S. L. P. 228 Tel 2820295 MPANDA

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0757533898**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0755247496**
- **Mwandamizi Taaluma 0754837977**
- **Mwandamizi Malezi 0783451863**

## KIAMBATA "A"

1. SKETI YA DARASANI.



2. SKETI YA KUSHINDIA



3.BLAUZI YA KUSHINDIA



# KIAMBATA "B"

## . TAALUMA: -

Kwa kuwa shule ina uhaba wa vitabu, inashauriwa mwanafunzi aje na vitabu vitakavyomsaidia kwa masomo husika kati ya vilivyoorodheshwa hapa chini:-

### I. VITABU VYA KEMIA: -

1. Jain s.k (2006) *Conceptual Chemistry XI ,4th edition*. Chand, New delhi India
2. Ngaiza lusima (2014) *Atomic Structure and Bonding*. Hopegen company ltd. Dar es salaam. Tanzania
3. Ngaiza lusima (2014*) Physical Chemistry*. Hopegen Company Ltd. Dar es salaam. Tanzania
4. Ngaiza lusima (2014) *Inorganic Chemistry*. Hopegen Company Ltd. Dar es salaam. Tanzania
5. Ngaiza lusima (2014) *Environmental and Soil Chemistry*. Hopegen Company Ltd. Dar es salaam. Tanzania.
6. E. Ramsden (2001) *Calculations for A-level chemistry*.

### II. VITABU VYA BIOLOJIA: -

1.Gleen and Toole (1999). *Understanding Biology 4th Edition*.Stanlye Thomes LTD UK.

2. Kent M. (2013). *Advanced Biology*.Oxford University Press LTD 2nd Edition

3.Aggarwal S. (2017). *A text book of CBSE.Biology for Class XI*.Nijra Publishers and Printers PVT.LTD

4. Verma P. S and Pandey BP (2012). *S. Chands Biology for class VI*.Chand and Company LTD.New Delh

5. Verma P. S and Pandey BP (2012). *S. Chands Biology for class VII*.Chand and Company LTD.New Delh

6. Taylor etal (1997) *Biological Science.3rd Edition*, Cambridge university Press LTD.

7 T.I.E (2019) *Biology for Advanced Level Secondary School.Student's Book Form Six,* Dar es salaam, T.I.E

8. T.I.E (2019) *Biology for Advanced Level Secondary School.Student's Book Form Five*, Dar es salaam, T.I.E

### III. VITABU VYA HISTORY: -

1. Bigirwamungu, J & Deogratias M. (2015) *Understanding African History*,Paper 1, New Version, Mikumi Publishers.

2. Kato, A.K. (2012) *Mastering Advanced Level History Book*, Mwanza, Mweas Book Publishers

3. Kato, A.K (2012) *Mastering Advanced Level History Book 2*, Mwanza, Mweas Book Publishers

4. Samwel, S & Stephen. O (2008) *World History Advanced Level*, Dar es salaam, Nyambari Nyangwine Publishers.

5. Shibitali, C.K (2017) *Contemporary Historical Events*, Third Edition, Dar es salaam, Che Guevara Investment.

6. Yassin,S.(2015) *Essentials in Advanced Level History Paper 1*, Dar es salaam, Ahmaddiya Printing Press.

7. Yassin,S.(2015) *Essentials in Advanced Level History Paper 2*, Dar es salaam, Ahmaddiya Printing Press .

8. Tanzania Institute of Education (2010) *History for Secondary Schools Form Five*, Dar es Salaam, T.I.E.

9. Tanzania Institute of Education (2010) *History for Secondary Schools,* Form Five, Dar es Salaam, T.I.E

**IV. VITABU VYA KISWAHILI**: -

1. Masebo, J.A & Nyangwine. N (2010) *Tahakiki Kidato cha 5& 6.* Nyambari Nyangwine Publisher, Dar es Salaam.
2. Mwansoko, H.J.M (1996) *Kitangulizi cha Tafsiri*, TUKI – Dar es Salaam.
3. Kihore. Y.M na Wenzake (2001) *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu, Sekondari na Vyuo*; TUKI Dar es Salaam.
4. Massamba, D.P.B na Wenzake (2001) *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu, Sekondari na Vyuo*; TUKI Dar es Salaam.
5. Saluhaya, M.C (2010) *Nadharia ya Lugha Kidato cha 5 & 6.* S.T.C Publishers- Dar es Salaam.
6. Masebo.J.A & Nyangwine, N (2009) *Nadharia ya Lugha kidato cha 5 & 6* . Nyambari Nyangwine Publishers. Dar es Salaam.
7. Masebo, J. A & Nyangwine, N. (2008) *Nadharia ya Fasihi Kidato cha 5 & 6*, Nyambari Nyangwine Publishers. Dar es Salaam.

**V. VITABU VYA UCHUMI: -**

1. C.M. Ambilikile – *Advanced level paper two and professional studies*

2.Economic 2*; Advanced levels paper two and professional studies*

*3.Undestanding Economics* (Remed H. Chegee.M)

**VI. VITABU VYA PHYSICS: -**

1.Mehta, R. and V. K Mehta (2009) *"Principles of Physics for Class XI*" New Delhi, S.Chand and Company Ltd.

2. Nelcon, M and P. Parker (1995) *"Advanced level Physics''* 07th Edition, London, Heinmann Educational books.

3. TIE (2019) "*Physics for Advanced Level Secondary Schools*, Form Five, Dar es salaam, TIE.

**VII. VITABU VYA ADVANCED MATHEMATICS**

1.Mathematics, For Class XI, Volume I, S. CHAND
2.Mathematics, For Class XI, Volume II, S. CHAND
3.Mathematics, For Class XII, Volume I, S. CHAND

4.Mathematics, For Class XII, Volume ii, S. CHAND

5.Pure Mathematics 1, 3rd edition, Backhouse, J.K, Houldsworth, S.P.T, B.E.D(1985)

6.Pure Mathematics 2, 3rd edition, Backhouse, J.K, Houldsworth, S.P.T, B.E.D(1985)

## VIII. VITABU VYA JIOGRAFIA: -

1. Pritchard J.M. (1979*) "Africa a study Geography for Advanced students"* London, Longman.

2.Msabila D. T (2003) *"Success in Geography climatology and Soil Science",* Dar es salaam, Afroplus Industries L.T.D

3. Prichard J.M. (1990) *"Practical Geography for Africa"* Longman.

4. Kamili, 2, *Physical Geography for Africa*, Dar es salaam, Afroplus Industries.

5.Msabila D.T. *Physical Geography*, Dar es slaam Nyambari Nyangwine Publishers.

6 Msabila D.T. (2006) *Human and economic Geography* (Advanced level paper 2) Nyambai Nyangwine publishers.

## IX. VITABU VYA SOMO LA KIINGEREZA

1. Ndambo,G.S & Kinunda, J.E. (2017). *Advanced Level English Language 1*, Form 5&6. Dar es salaam: Nyambari Nyangwine Publishers.

2. Kadeghe, M. (2010), *The Real English Textbook for Advanced Level*, Form Five, Dar es salaam, Jamana Printers Limited.

3. Kadeghe, M. (2010) *The Real English Textbook for Advanced Level*, Form Six. Dar es salaam, Jamana Printers Limited.

4. Asheli, N. (217) *Advanced Level English Language Structure & Stylistics*, Dar es salaam, APE publishers Ltd.

5. Lyi Kwei Armal, *the beautiful one are not yet born.*

6. Chunua Achebe, *A man of the people*

7. Heinrich Ibsen, *An Enemy of the people*

8. Ngungi wa Thiongo, *I will merry when I want*.

## X. VITABU VYA ACCOUNTANCY.

1.Wood.F & Sangster (2018) *"Business accounting"* 14th edition, UK,

Pearson publishers.

2.Saleem, N. A (2012) *"Advanced Financial Accounting Simplified*"

Volume II, Nairobi.

3.Saleem N.A, (2014) *"Accounting Simplified"* latest edition, Nairobi,

4. Goyar V.K, (2014) *"Financial Accounting"* Kalyani publishers

5.Chandi S & Pillai Bagavathi (2012). *"Fundamentals of Advanced Accounting"*, Delhi publishers.

**XI.VITABU VYA COMMERCE**.

1. Saleemi, N.A (2014) *Commerce Simplified for East Africa*, Rvised and Updated, Nairobi, Saleemi publications Ltd.

**XII. GENERAL STUDIES: -**

1. Bigirwamungu, J & Deogratias M.5th Edition (2019) *Understanding Advanced Level General Studies*, Dar es salaam, Mikumi Publishers.
2. Tanzania Institute of Education (2010), *General Studies for Secondary Education*, Dar es Salaam, T.I.E

# KIAMBATA 'C'

## SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA MPANDA

## MEDICAL EXAMINATION FORM

To be completed by a medical officer in respect to all form of entrants

Student's full name ……………………………………………………………………………….

Age ……… Years ……… Sex ………………….

Blood count (red and whites) ……………………………………………………………….

Stool examination …………………………

Urine analysis

Syphilis and other venereal diseases test ……………………………………………

T.B test ……………………………………
EyeTest……………………………………………………………………………
Ears…………………………………………………………………………..

Abdomen…………………………………………………….

Urine for plant ……………………………………

Test for pregnancy ……………………………………………………………………………….

ADDITIONAL INFORMATION

Defects, impotents (e.g., arms, legs etc) infections, chronic or family diseases etc

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

I certify that the named above is fit to pursue further studies in agricultural/domestic education

Station ……………………………………………….....................

Signature …………………

Date.………………………………………………designation……………………………

## KIAMBATA ‘D’

**SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA MPANDA**

**HISTORIA YA WAZAZI NA MTOTO ALIYECHAGULIWA KUJIUNGA NA SHULE HII: -**

**A. WAZAZI/WALEZI**

1. Jina la Baba ………………………………………………… Hai/Si hai.
2. Jina la Mama …………………………………………… Hai/ Si hai.
3. Kama Baba si hai jina la mlezi ni ……………………………………………………………
4. Kazi/Shughuli ya Mzazi/Mlezi ……………………………………………………………….
5. Anwani ya Mzazi/Mlezi………………………………………………………………
6. Uraia wa wazazi
   -Baba Mtanzania/Si Mtanzani.

   -Mama Mtanzania/ Si Mtanzania.
7. Wakati wa likizo mtoto/Mwanafunzi anatakiwa arudi nyumbani kwao alikotoka ambako ni …………………………………………………………………………
8. Jina la mtu aendako …………………………………………………….
9. Uhusiano na mtoto/mwanafunzi.……………………………………….

**SAHIHI YA BABA/MLEZI…………………………TAREHE ………………….**

**SAHIHI YA MWANAFUNZI …………………………TAREHE …………………**

**N.B. KILA MWANAFUNZI ANAPOKUJA AJE NA NAKALA YA CHETI CHAKE CHA KUZALIWA NA NAKALA YA KADI YA NIDA YA MZAZI, KAMA MZAZI HANA KADI YA NIDA MWANAFUNZI AJE NA NAMBA YA NIDA.**

# KIAMBATA "E"

**SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA MPANDA**

## FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE

Mimi ………………………………………………………………………… nimesoma kwa makini maagizo yote na ninatambua kuwa kuchaguliwa kwangu kuingia shule ya Sekondari ni bahati na zawadi kubwa kwa kuwa wengi wamekosa nafasi si kwa kuwa wameshindwa ila kwa sababu ni chache.

Hivyo nakubali kujiunga na shule ya Mpanda Sekondari ya Wasichana. Nitatii na kufuata sheria na taratibu zote za Shule.Na ninaahidi kwamba sitashiriki katika migomo ya aina yoyote,kuanzisha au kushiriki fujo na kujihusisha na makosa ya jinai. Nitajitahidi kufanya kazi/kusoma kwa juhudi na maarifa na nitajitahidi kushirikiana na wenzangu daima.

Nitalinda hadhi/heshima ya Shule ya Mpanda Sekondari ya Wasichana na nitashirikiana na wenzangu kujenga misingi na historia nzuri ya shule.

(i).Tahasusi………. (ii). Uraia……………………. (iii). Kabila……………………

(iv)Dini……………………………

(vi)Tarehe ya kuzaliwa…………………………….

(Vii).Mahali ulipozaliwa: Kitongoji/mtaa……………………… Kijiji………………….
Kata………………………… Tarafa…………………
Wilaya/Mji………………………… Mkoa…………………

(viii). Taarifa za Shule ulizosoma:- Msingi…………………Sekondari…………………

Tarehe……………………. Sahihi ya mwanafunzi……………………………………………

Mimi Mzazi/ Mlezi ……………………………………………………….,Nimeshuhudia mtoto wangu …………………………………….. akikubali kwa hiari kujiunga na shule hiyo, ninaamini mtajitahidi kumfunza na kumlea vizuri. Mimi pia naahidi kushirikiana nanyi kikamilifu katika kumlea binti yangu naamini tutakuwa tunawasiliana.

Tarehe………………………………… Sahihi ya Mzazi/Mlezi…………………………

**BAADHI YA VIFAA VINAVYO PATIKANA KATIKA DUKA LA SHULE NA BEI ZAKE.**

## 1. STATIONARY

| S/NO | VIFAA | BEI |
|---|---|---|
| 1. | RIM PAPER (A4) | TSH. 15,000/= |
| 2. | COUNTER BOOK QUIRE 2 | TSH. 2,500/= |
| 3. | COUNTER BOOK QUIRE 3 | TSH. 3,500/= |
| 4. | COUNTER BOOK QUIRE 4 | TSH. 4,500/= |
| 5. | SCIENTIFIC CALCULATOR | TSH. 40,000/= |
| 6. | DAFTARI ZA MSOMI | TSH. 1,000/= |
| 7. | PENI | TSH. 200/= |
| 8. | MKEBE (MATHEMATICAL SET) | TSHS. 2,500/= |

## 2. VIFAA VYA USAFI

| S/NO | VIFAA | BEI |
|---|---|---|
| 1. | JEMBE NA MPINI | TSH. 7,000/= |
| 2. | BRUSH NGUMU | TSH. 3,000/= |
| 3. | BRUSH LAINI (SOFT BROOM) | TSH. 3,000/= |
| 4. | SQUIZER | TSH. 3,000/= |
| 5. | NDOO NDOGO LITA 10 | TSH. 4,000/= |
| 6. | FAGIO ZA CHELEWA | TSH. 2,000/= |
| 7. | BESENI LA KUFULIA NGUO | TSH. 4,000/= |

## 3. NGUO

| S/NO | NGUO | BEI |
|---|---|---|
| 1. | SHATI TOMATO | TSH. 10,000/= |
| 2. | SHUKA NYEPESI KIJANI KIBICHI | TSH. 12,000/= |
| 3. | NETI | TSH. 8,000/= |
| 4. | VIATU (SIMPLE ZA BILA KAMBA) | TSH. 12,000/= |
| 5. | NGUO ZINGINE MUHIMU ZINAPATIKANA | - |
| 6. | TRACK SUIT | 22000/= |

## 4. VYOMBO VYA CHAKULA

| S/NO | VIFAA | BEI |
|---|---|---|
| 1. | SAHANI ZENYE MFUNIKO | THS. 3,000/= |
| 2. | VIKOMBE | TSHS 1,000/= |
| 3. | KIJIKO | TSHS. 500/= |

**NB:** *Dukani pia kuna huduma ya **KIFEDHA** kama vile **NMB WAKALA**, kwa wale wanaotaka kuwafungulia Watoto wao akaunti za benki*